**Haki Zangu kama Mshiriki wa WIC.**

- Sheria za kujiunga na WIC ni sawa kwa kila mtu bila kujali mbari, rangi, asili ya taifa, umri, ulemavu au jinsia.
- Madhumuni ya WIC ni kutoa taarifa kuhusu lishe, unyonyeshaji na vyakula bora na kuniwezesha kuwasiliana na huduma nyingine yoyote ya afya au ya jamii ninayoweza kuhitaji. Ninahimizwa kushiriki katika huduma hizi.
- Wataalamu wa afya wa WIC watashirikiana nami kuunda malengo ya lishe ili kusaidia mtindo wa maisha wenye afya bora.
- Ikiwa nitahamia jimbo jingine, nitafahamisha WIC na watanipa karatasi za uhamisho ili huduma zangu za WIC ziendelee katika jimbo hilo jingine.
- Ninaweza kuomba Usikilizaji Tena wa Kesi wa Haki ikiwa mfanyakazi wa WIC ataniambia kwamba siwezi kujiunga na WIC na sikubali. Nina siku 60 kutoka wakati wa kupokea barua kuhusu ustahiki wangu kuandikia barua au kuwasiliana na ofisi yangu ya WIC ya karibu na kuomba nipewe

**Majukumu Yangu kama Mshiriki wa WIC:**

- Kushiriki katik zaidi ya Mpango mmoja wa WIC (ndani ya jimbo au nje ya jimbo) ni haramu na kutasababisha kusimamishwa kwangu kwenye mpango.
- Nitaruhusu uchunguzi wa afya wa WIC kwa waombaji wote wa WIC katika familia yangu. Uchunguzi wa afya wa WIC ni pamoja na kujibu maswali ya afya na lishe, kupima kimo, uzani na kuchunguza ikiwa damu ina anemia. Hii husaidia WIC kutoa fidia ambazo zinakidhi mahitaji ya familia yangu.
- Nitakuja kwenye miadi yangu au kupiga simu mapema ikiwa siwezi kufika kwenye miadi yangu.
- Nitaarifu WIC kuhusu mabadiliko yoyote makubwa yanayoweza kutokea kama vile taarifa zangu za mawasiliano, mabadiliko ya jina na mabadiliko ya malezi ya watoto ninaowatunza ambao wanapokea huduma za WIC.
- Nitawaheshimu na kuwapa hadi wafanyakazi wa WIC, wafanyakazi wa stoo ya chakula na mali. Ninaelewa kwamba mimi au yeyote kati ya mawakili wangu, anaweza kufunga fidia za chakula changu cha WIC kwa kutusi, kunyanyasa, kutisha au kumdhuru mfanyakazi wa WIC, mteja mwingine wa WIC au mfanyakazi wa stoo ya chakula.
- Nitanunua tu vyakula vilivyoidhinishwa ambavyo vimeorodheshwa kwenye orodha ya fidia yangu ya chakula cha WIC kwa kadi ya eWIC niliyopewa.
- Nitatumia vyakula vya WIC kwa watu walio kwenye mpango pekee. Ninaelewa kwamba vyakula hivi vya WIC vinatolewa ili kuendeleza na kusaidia hali njema ya lishe ya mtu huyo na kusaidia kukidhi ulaji unaopendekezwa wa virutubishi au vyakula muhimu.
- Sitabadilisha, kuuza, kuhamisha wala kubadilishana, au kujaribu kubadilisha, kuuza, kuhamisha wala kubadilishana, chakula/fomula yoyote au fidia nilizopewa. Sitaruhusu mtu mwingine yeyote kubadilisha, kuuza, kuhamisha wala kubadilishana, au kujaribu kubadilisha, kuuza, kuhamisha wala kubadilishana, chakula/fomula yoyote au fidia nilizopewa.
- Nitahifadhi stakabadhi zote za duka kw miezi mitatu ya chakula au fomula ninayonunua kwa fedha ambazo si za WIC zinazofanana na zile zilizotolewa na WIC ikiwa ninakusudia kuuza, kubadilisha au kuwapa watu bidhaa hizi. Hili ni linafanyika ili niweze kuthibitisha kuwa hazikununuliwa kwa fedha zangu za WIC.

**Kama Mshiriki wa WIC ninaelewa:**

- Lazima nitume ombi tena mwishoni mwa kipindi cha uthibitishaji na kutathminiwa tena kwa ajili ya ustahiki wa mpango.
- WIC haitoi chakula au fomula yote inayohitajika kwa mwezi kwa sababu WIC ni mpango wa kujaliza.
- Ikiwa sijapewa fidia za chakula kwa miezi minne mfululizo, nitasimamishwa kwenye mpango.
- Department of Health and Human Services (HHS) inaweza kuidhinisha ushiriki wa taarifa za WIc na mipango mahususi ya afya na elimu. Mipango hii inaweza kutumia taarifa hizi kuamua ustahiki wangu wa mipango yao; kunipa taarifa kuhusu mipango hiyo na kurahisisha mchakato wa utumaji ombi; kuboresha afya, elimu au ustawi wangu ikiwa tayari nimejiandikisha katika mipango yao; na kuhakikisha kwamba mahitaji ya huduma ya afya yangu yamekidhiwa. Taarifa hizi zitatumiwa na mawakala wa WIC na mashirika ya umma katika usimamizi wa mipango yao inayotumikia watu wanaostahiki Mpango wa WIC. Ninaelewa kuwa HHS inaweza pia kuidhinisha ushiriki wa taarifa zangu za WIC inavyohitajika au ilivyoidhinishwa na sheria ya serikali kuu au jimbo. Ninaweza kuomba orodha ya mipango ya HHS ambayo taarifa zangu za WIC zinaweza kushirikiwa nayo kama zinavyopatikana katika Sera ya WIC ya "Usiri wa Taarifa za Mshiriki".

Nimeshauriwa kuhusu haki na majukumu yangu chini ya Mpango. Ninathibitisha kwamba taarifa ambazo nimetoa kwa ajili ya uamuzi wa ustahiki wangu ni sahihi, kadri ya ufahamu wangu. Fomu ya uthibitishaji inawasilishwa kuhusiana na upokeaji wa usaidizi wa Serikali Kuu. Maafisa wa mpango wanaweza kuthibitisha taarifa kwenye fomu hii. Ninaelewa kwamba kutoa taarifa za uongo au za kupotosha au kuwasilisha taarifa visivyo, kuficha, au kuzuia maelezo sahihi kunaweza kusababisha kulipa shirika la Jimbo, kwa pesa taslimu, thamani ya fidia za chakula nilizopewa visivyo na kunaweza kunifanya nishtakiwe kwa kosa la raia au uhalifu chini ya Sheria ya Jimbo na Serikali Kuu.

Jin a la Mshiriki wa WIC aliyethibitishwa leo: ______________________________________

Sahihi ya mshiriki/mzazi/mlezi _________________ Tarehe: ____________________

Kwa mujibu wa sheria ya Serikali Kuu ya haki za kiraia na kanuni na sera za haki za kiraia za U.S. Department of Agriculture (USDA), taasisi hii hairuhusiwi kubagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya utaifa, jinsia (ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia), ulemavu, umri, au kulipiza kisasi kwa shughuli za awali za kuhusika katika haki za kiraia.

Taarifa za mpango zinaweza kupatikana katika lugha nyingine isipokuwa Kiingereza. Watu walio na ulemavu wanaohitaji njia mbadala ya mawasiliano kwa ajili ya taarifa za mpango (kwa mfano, Breli, maandishi ya herufi kubwa, ukanda wa sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani), wanapaswa kuwasiliana na jimbo husika au shirika la karibu linalosimamia mpango au Kituo LENGWA cha USDA kwa nambari (202)720-2600 (sauti na TTY) au wasiliana na USDA kupitia Federal Relay Service kwa nambari (800)877-8339.

Ili kuwasilisha malalamishi ya ubaguzi, Mlalamishi anapaswa kujaza Fomu ya AD-3027, Fomu ya Malalamishi ya Ubaguzi ya Mpango wa USDA ambayo inaweza kupatikana kwenye: https://www.usda.gov/sites/default/files/documents/ad-3027.pdf, kutoka kwenye ofisi yoyote ya USDA, kwa kupiga simu (866)632-9992 au kwa kuandika barua kwa USDA. Lazima barua iwe

na jina, anwani, nambari ya simu ya mlalamishi na maelezo ya maandishi kuhusu madai ya hatua ya kibaguzi kwa undani wa kutosha ili kumfahamisha Assistant Secretary for Civil Rights (ASCR, Katibu Msaidizi wa Haki za Kiraia) kuhusu asili na tarehe ya madai ya ukiukaji wa haki za kiraia. Barua au fomu au barua ya AD-3027 lazima iwasilishwe kwa USDA na:

(1) Barua: U.S. Department of AgricultureOffice of the Assistant Secretary for Civil Rights1400 Independence Avenue, SWWashington, D.C. 20250-9410; au
(2) Faksi: (833)256-1665 au (202)690-7442; au
(3) Barua pepe: program.intake@usda.gov

Taasisi hii ni mtoa huduma asiyebagua .